

MAKAO MAKUU

Ghorofa ya 4, Jengo la LAPF, Barabara ya Makole

S.L.P. 2857, Dodoma, Tanzania

Simu: +255-26 2329002-3; Nukushi: +255-26 2329005

Barua pepe: info@ewura.go.tz

Tovuti: <http://www.ewura.go.tz>

TANGAZO KWA UMMA

MWITO WA MAONI YA WADAU KUHUSU MAOMBI YA MAREKEBISHO YA BEI ZA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA KUTOKA MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA YA KARAGWE (KARAGWE WSSA) KWA MWAKA 2018/19

Maombi ya Mabadiliko ya Bei Na. TR-W-18-014-2018/2019

Mnamo tarehe 26 Oktoba 2018 Mamlaka ya Udhubiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ilipokea maombi yaliyokamilika kutoka Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira ya Karagwe (Karagwe WSSA) ya kutaka kurekebisha bei za huduma zake za maji safi kwa mwaka 2018/19. Majedwali namba 1 hadi 5 hapa chini yanaonesha mchangano wa bei za sasa na bei zinazopendekezwa

Jedwali Na 1: Bei za Sasa na Zinazopendekezwa kwa Wateja Wenye Dira (Shilingi kwa Uniti moja ya ujazo)

Kundi la Wateja	Bei za Sasa	Bei Zinazopendekezwa	
	2017/18	Mabadiliko (%)	2018/19
Majumbani	800	125%	1,800
Taasisi	1,000	100%	2,000
Biashara	1,025	144%	2,500
Magati	2,500	100%	5,000
Kuosha Magari	-		5,000
Ujenzi	-		5,000

Jedwali Na.2: Bei ya Sasa na Inayopendekezwa kwa Wateja wasio na Dira (Shilingi kwa Mwezi)

Kundi la Wateja	Bei za Sasa	Bei Zinazopendekezwa	
	2017/18	Mabadiliko (%)	2018/19
Majumbani	6,500	54%	10,000
Taasisi	9,500	163%	25,000
Biashara	10,000	150%	25,000
Kuosha Magari	-		30,000
Ujenzi	-		30,000

Jedwali Na.3: Tozo ya Huduma ya Sasa na Inayopendekezwa (Shilingi kwa Mwezi)

Kundi la Wateja	Tozo ya Sasa	Tozo Zinazopendekezwa	
	2017/18	Mabadiliko (%)	2018/19
Majumbani	800	25%	1,000
Taasisi	800	88%	1,500
Biashara	800	88%	1,500
Kuosha Magari	-		3,000
Ujenzi			5,000

Jedwali Na.4: Ada ya Maunganisho ya Huduma ya Maji ya Sasa na Inayopendekezwa (Shilingi kwa Maunganisho)

Kundi la Wateja	Ada za Sasa	Ada Zinazopendekezwa
	2017/18	2018/19
Majumbani	20% ya Gharama za Maunganisho	50,000
Taasisi		75,000
Biashara		75,000
Viwanda	-	75,000
Magati	-	75,000
Kuosha Magari	-	75,000
Ujenzi	-	75,000

Jedwali Na.5: Ada za Sasa na Zinazopendekezwa za Kurejeshwa Huduma Baada ya Kukatiwa (Shilingi/Kurejeshwa huduma)

Kundi la Wateja	Ada za Sasa	Ada Zinazopendekezwa	
	2017/18	Mabadiliko (%)	2018/19
Majumbani	10,500	0%	10,500
Taasisi	11,500	74%	20,000
Biashara	11,500	74%	20,000
Kuosha Magari	-	-	20,000
Ujenzi	-	-	20,000

Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Karagwe imeeleza kuwa bei na tozo zinazopendekezwa zitaiwezesha mamlaka kulipa gharama za uzalishaji na usambazaji wa maji, matengenezo katika mtandao wa usambazaji wa maji, uchakavu wa miundombinu, ununuzi wa vifaa na uwekezaji ili kuboresha utoaji wa huduma na kuongeza wigo wa wateja.

Kwa mujibu wa kifungu Na. 19 (2) (b) cha Sheria Na. 414, kutakuwa na Mkutano wa Taftishi siku ya **Jumatano, tarehe 21 Novemba 2018 katika Ukumbi wa Mikutano wa Angaza** uliopo katika Mji wa Kayanga (Karagwe) kuanzia saa **4:00 asubuhi**. Lengo la mkutano huo ni kwa ajili ya kupata maoni ya wadau ikiwa ni pamoja na Baraza la Ushauri la Serikali na Baraza la Ushauri la watumia Huduma zinazodhibitiwa na EWURA, wateja wa Mamlaka ya Maji Karagwe na wananchi wote kwa ujumla kuhusu uhalali wa bei zinazopendekezwa.

Wadau wanaopenda kutoa maoni kwa maandishi wanaombwa kufanya hivyo kwa kutuma maoni yao kwa Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa EWURA kwa anuani iliyoonesha hapo juu **ifikapo tarehe 28 Novemba 2018**. Maelezo zaidi yanaweza kupatikana katika ofisi za **EWURA KANDA YA ZIWA, GHOROFA YA NNE, JENGO LA PPF; BARABARA YA KENYATTA, MWANZA** au **OFISI ZA MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA KARAGWE**

Imetolewa na:
Kaimu Mkurugenzi Mkuu
Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji
(EWURA)

5 Novemba 2018